KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Mch. Mark Finley – Mwenyekiti Msaidizi wa Konferensi Kuu

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la 9, Mei 22 – 28, 2020

WAKATI WA KUUCHUNGUZA MOYO

Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu;
Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele – Zaburi 139:23, 24

Miaka mingi iliyopita, mwanzoni mwa huduma yangu, nilialikwa kuendesha juma la Mkazo wa Kiroho katika shule moja ya msingi wa Kikristo. Juma lilipokuwa nikiendelea niligundua kuwa walimu wawili walikuwa katika mgogoro mzito. Mitazamo yao hasi kila mmoja kwa mwenzake mara kwa mara iliibuka kwenye vikao vya wafanyakazi. Ikiwa mmoja alipendekeza wazo fulani, yule mwingine alilipinga. Wote wawili walipokuwepo kwenye mkutano, hali ya hewa ilijawa na mvutano. Ilikuwa wazi kwamba hawakupendana kabisa.

Mwishoni mwa juma, nilihubiri juu ya ombi la Kristo la upatanisho la Yohana 17. Yesu alikuwa karibu kuwaacha wanafunzi wake. Muda mfupi uliofuata angesalitiwa na kusulubiwa. Angefufuka toka kaburini na kupaa kwa Baba yake. Ombi lake la dhati linaakisi kile kilichokuwa ndani ya moyo wake. Linadhihirisha kile kilichokuwa akilini mwake. Mwokozi alikuwa na wasi wasi juu ya umoja wa kanisa. Aliomba, “Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma - Yohana 17:21. Kristo alitamani kuwa ugomvi, wivu, kugombea ukuu, na mapambano miongoni mwa wanafunzi wake vikome. Aliomba kwamba umoja wao, pamoja na tofauti zao, zingeudhihirishia ulimwengu nguvu ya upendo wake.

Nilipokuwa nawashuhudia hawa wanafunzi na walimu juu ya shauku hii ya moyo wa Yesu, jambo fulani la ajabu lilitokea. Usiku wa mwisho wa juma letu la Mkazo wa Kiroho, tulipanga tuwe na huduma ya kutawadhana miguu na meza ya Bwana. Roho Mtakatifu alitamalaki. Mungu alileta mguso wenye nguvu. Wale walimu wawili waliopitia utengano mkubwa kiasi kile walipiga magoti wakikabiliana. Walikumbatiana, wakaungamiana mitazamo yao hasi na wakaombeana.

Wa Yesu walipitia toba tamu na unyenyekevu sawa na huo katika zile siku 10 walizokaa chumba cha juu zilizotangulia Pentekoste. Katika siku hizo kumi, wanafunzi waliungamiana tofauti zao ndogo ndogo miongoni mwao. Waliungama juu ya wivu wao na kiburi. Na mioyo yao ilijawa na upendo kwa Kristo aliyetoa kwa ajili yao. Walitamani wangeishi miaka ile mitatu tena wakiwa pamoja.

Je! Umewahi kujisikia hivyo? Umewahi kutamani urudi nyuma na kurekebisha makosa yako yaliyopita? Tunapouona wema wa Mungu wa upendo na kuitazama haki ya tabia yake, tunautambua udhaifu wetu, kushindwa kwetu na dhambi zetu. Katika nuru angavu ya upendo wake usio na masharti na ukamilifu, mioyo yetu inanyenyekeshwa. Tunaongozwa kwenye ungamo la kina na toba. Tunamlilia ili tupate wokovu na haki ambayo ni yeye pekee awezaye kuitoa. Tunapoguswa na utakatifu wake, tunalia pamoja na nabii Isaya, “Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu” (Isaya 6:5). Kila mara kujichunguza kunaweweza kusiwe ni uzoefu wa kupendeza, lakini ni jambo la muhimu kabisa. Tunapojichunguza tunamwomba Mungu, “Je! Kuna kitu fulani maishani mwangu ambacho hakipatani na mapenzi yako?” Tunaomba, “Bwana, ifunue mitazamo isiyofanana na Yesu iliyo kwenye kina cha roho yangu”

Lengo la Mungu katika mchakato huu ni kutuongoza karibu zaidi na yeye. Hataki tuanguke chini katika hatia au tujazwe na majuto ya maisha yetu yaliyopita. Lengo lake ni kutuongoza "katika njia ya milele." Ingawa ni jambo jema kujichunguza kwa wazi juu ya maisha yetu wa kiroho, sio jambo jema kutafakari makosa ya maisha yetu yaliyopita. Kuyatafakari makosa yetu na kulenga kwenye makosa yetu kwa muda mrefu hutukatisha tamaa tu.

Daima kumbuka kuwa Mungu wetu ni mkubwa kuliko makosa yetu na ni mkuu kuliko kushindwa kwetu. Kwa hakika tunatakiwa kuijua hali yetu kwa uaminifu – lakini ni muhimu zaidi kuijua neema yake. Kuuelewa udhaifu wetu hutuandaa kupokea uwezo wake. Kuielewa hali yetu ya dhambi hutuandaa kuipokea haki yake. Kuelewa ujinga wetu hutuandaa kuipokea hakima yake. Kusudi la usadikisho wa Roho Mtakatifu ni kutuongoza kwa Yesu. Tunapotambua dhambi zetu na makosa yetu kupitia mchakato wa kujichunguza, tunaweza kumshukuru Mungu kwa vile Roho Mtakatifu anatuongoza karibu zaidi na Yesu, na kama matokeo tunakuwa karibu zaidi sisi kwa sisi. Uwezo wa mvuto wa Roho Mtakatifu unatuandaa kumpokea Roho kwa wingi katika nguvu ya mvua ya masika. Lakini kabla ya kututengeneza, Mungu ni lazima atuvunje kwanza. Kabla hajatujaza, ni lazima atumwage kwanza. Kabla ya kutawala mioyoni mwetu, ubinafsi ni lazima utupiliwe mbali.

Maswali ya Moyoni: Moyo wako uko wapi leo? Je! Umepitia uzoefu karama tamu ya toba? Kama ndio, Je! Maisha yako yapo tofauti na yalivyokuwa kabla? Je! Umepitia uzoefu wa neema ya Mungu kwa namna mpya? Umejifunza kuwapa watu wengine neema hiyo?

Changamoto Hai Moyoni: Mwombe Mungu ayafunue mambo ya maisha yako ambayo yawezekana yanakupotezea muda, usikivu wako, na au yanachepusha mapenzi yako kutoka kwa Yesu. Unapotafakati Isaya 59:1-2, na 1 Yohana 1:9, Sali na umwombe Mungu afunue uvunjifu wo wote wa kiroho maishani mwako. Omba kwamba auondoe na akujaze Roho Mtakatifu.

"Toba hujumuisha huzuni ya moyo kwa ajili ya dhambi na kugeukia mbali dhidi yake. Hatutaweza kuikataa dhambi tusipouona ubaya wa dhambi; tusipoiacha kutoka moyoni, hakutakuwa na badiliko halisi katika maisha. Wapo wengi wanaoshindwa kufahamu asili ya kweli ya toba. Umati wa watu unahuzunika kwa sababu wametenda dhambi na hata wanafanya matengenezo ya nje kwa sababu wanaogopa kwamba matendo yao mabaya yatawaletea mateso wao wenyewe. Lakini hiyo sio toba kwa maana ya Biblia... (kama ilivyokuwa kwa Esau, Baalamu, Yuda Iskariote, na hata Farao). Kinyume chake Daudi aliuona ubaya wa uasi wake; aliona unajisi wa roho yake; aliichukia dhambi yake. Hakuomba tu kwa ajili ya msamaha, lakini kwa usafi wa moyo." – Steps to Christ pp. 23-025

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:

- Ellen White, *Steps to Christ,* Ch. 3 *"Repentance"*
- Mark Finley, *10 Days in the Upper Room*

Siku ya 57, Ijumaa, Mei 22, 2020

Taarifa za Sifa:

- Jinia Y., anasema: “Ninamsifu Mungu kwa ajili ya huduma za vyombo vya habari. Hotuba na shuhuda tunazoweza kuzitazama kwa njia ya mtandao zinanisaidia kukabiliana na maumivu ninayoyapata wakati huu wa kutengwa.”

- Yvonne L., anasema, “Nilipokea simu kupitia kazi yangu ili kumsaidia mtu fulani ambaye nilikuwa sijawahi kumwona kabla. Nililiombea jambo hilo kisha nikaenda kumwona mtu huyu. Kupitia maongezi iligundulika kwamba huyu mtu aliwahi kuwa kiongozi Mwadventista aliyekuwa ameliacha kanisa. Niliweza kuomba naye na alikiri kuwa alihisi Roho Mtakatifu akimwita kurudi. Ninamsifu Mungu ambaye si tu hutoa fursa za kushuhudia, lakini pia huelekeza namna ya kuitikia.”

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** maeneo ambako Covid-19 inaelekea kuibuka tena kama vile Wuhan, China na miji mingine na mikoa ya China.

- **Ombea** walimu Waadventista katika shule za serikali nchini Thailand. Kuna uwezekano mkubwa shule zitakapofunguliwa tena, serikali itapanga madarasa yafundishwe siku za Jumamosi ili kufidia muda uliopotea. Ombea imani imara ya walimu ili wasimame kama Danieli na rafiki zake watatu walivyosimama.

- **Ombea** vikundi vidogo, makanisa ya nje, na mikutano ya injili iliyoibuka nchini Papua New Guinea kwa sababu ya kufungwa kwa makanisa

- **Ombea** kituo cha huduma ya kupasha joto cha Kanisa la Waadventista wa Sabato Omega, kule New Haven, Connecticut, Marekani, ambacho kinahudumia watu wasio na makazi katika kukabiliana na amri ya kujitenga na jamii wakati huu wa janga la Covid-19.

Siku ya 58, Jumamosi, Mei 23, 2020

HERI MASKINI

Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao – Mathayo 5:3

"Wale wanaojua kwamba hawawezi kujiokoa wenyewe, au wao wenyewe hawawezi kufanya tendo lo lote la haki., ni wale wanaoukubali msaada anaoweza kutoa Kristo. Hao ndio maskini wa roho, ambao alitamka kuwa wana heri. Anaowasamehe Yesu, huwapa toba kwanza, na ni kazi ya Roho Mtakatifu kuthibitisha dhambi. Wale ambao mioyo yao imeguswa kwa ushawishi wa Roho wa Mungu huona kuwa hakuna cho chote chema ndani yao. Wanaona kwamba yote waliyowahi kufanya ni mchanganyiko wa ubinafsi na dhambi. Kama yule mtoza ushuru maskini wanasimama mbali, hawathubutu kuinua macho yao mbinguni, na wanalia, 'Mungu unirehemu mwenye dhambi'. . . Wote wenye ufahamu wa kina cha umaskini wa roho zao, wanaojihisi kuwa hawana cho chote chema ndani yao, wanaweza kupata haki na nguvu kwa kumtazama Yesu. – Thoughts from The Mount of Blessing, pp. 7-8

Maswali ya Moyoni: Kujihesabia haki – mtazamo unaosambaa na mara nyingi bila kujua, unatudanganya ili tufikiri na kujisikia kuwa sisi ni wema – ni kikwazo kubwa sana katika kuupokea kiukweli wokovu binafsi katika Yesu. Tunapotambua umaskini wetu kiroho, hitaji letu la kumpata na kutambua umaskini wetu kiroho, hitaji letu la kumpata la Yesu maisha yetu yote, na kama matokeo yake kumtumainia yeye pekee, wakati hadi wakati, kwamba atatuponya kikamilifu dhidi ya kila dalili ya ubinafsi, ndipo tutakapoweza kuwa na uhakikisho wa wokovu. Kwa nini leo, usije kwa Yesu kama ulivyo, ukiwa na nafsi yako yenye dhambi, iliyovunjika? Kwa nini usidai tu damu yake, maisha yake na mauti yake, kama njia ya wokovu? Kwa nini usimwombe ang'oe hali yote ya kujitegemea iliyo bado moyoni mwako na kuibadilisha na imani katika uweza wake kukuokoa, na kukupatia nguvu kutenda matendo mema yanayosukumwa na upendo usio na ubinafsi?

Taarifa za Sifa:

- Nolubabalo D., anasema "Asante Bwana kwa mkono wako kwa ajili ya Afrika. Asante kwa ulinzi wako. Asante kwa kuwatunza watoto wangu ninapokuwa sipo. Unastahili sifa zote."
- Philippe M., anasema "Katika mji wetu wa Kananga, hakukuwa na matangazo ya redio kabla ya mazuio ya Covid-19, lakini wakati huu wa zahama tunarusha matangazo manne kila juma kupitia vituo vinne vya redio mahalia. Tunamshukuru Mungu kwa hilo!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** Yesu akutakase dhidi hali yote ya kujihesabia haki na akupatie utambuzi wa hitaji lako kubwa la kila siku na la maisha yote la kumhitaji yeye.
- **Ombea** wainjilisti kule Afrika ya Kusini wanaopambana na masuala mbali mbali ya kiafya na msongo. Ombea ili waponywe na kuwezeshwa kupata njia za kuhubiri injili hata sasa.
- **Mwombee** Kaka Samuel S. anasumbuliwa na maumivu makali sehemu ya chini ya mwili wake na madaktari hawajui tatizo ni nini. Pia mwombee dada Tabitha N. aliyepimwa na kugundulika kuwa anatundu katika moyo wake na yupo kwenye maumivu makali. Ombea wapone na pia uponyaji wa wengine wengi wanaoteseka muda huu.
- **Ombea** Kituo cha Huduma ya Wachina kule Jakarta, Indonesia wanapoendelea kuendesha mikutano ya injili kwa njia ya mtanmdao kila Sabato tangu Mei 9 hadi Juni 20, 2020. Mkutano wa kwanza ulivuta zaidi ya watazamaji 3000 na zaidi ya 260 kati yao walijiandikisha kwenye masomo ya Biblia.

Siku ya 59, Jumapili, Mei 24, 2020

MAOMBOLEZO YAMEVUNJIKA

Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika – Mathayo 5:4

"Maombolezo yanayoletwa mbele yetu hapa ni huzuni ya kweli ya moyo kwa ajili ya dhambi...Na mtu anapovutwa kumtazama Yesu aliyeinuliwa msalabani, anatambua hali ya dhambi ya ubinadamu. Anaona kwamba ni dhambi zilizompiga na kumsulubisha Bwana wa utukufu. Anaona kuwa, wakati alikuwa amependwa kwa upendo usiosemeka, maisha yake yamekuwa daima uwanja wa ukosefu wa shukrani na uasi. Amemwacha rafiki yake kipenzi na kuipuuza zawadi bora zaidi ya mbinguni. Yeye mwenyewe amemsulubishwa Mwana wa Mungu kwa shimo la dhambi lililopana na jeusi na refu, na anaomboleza akiwa amevunjika moyo. Maombolezo kama hayo'yatafarijiwa.' Mungu hutufunulia hatia yetu ili tumkimbilie Kristo, na kwa njia yake tuwekwe huru dhidi ya kongwa la dhambi, na kufurahia katika uhuru wa mwana wa Mungu. Katika toba ya kweli tunaweza kuja chini ya msalaba, na pale tukaacha mizigo yetu." – Thoughts from The Mount of Blessing, pp. 9-10

Maswali ya Moyoni: Umewahi kutenga muda na kutambua kikamilifu kile Yesu alichofanikisha kwa ajili yako katika yale masaa ya giza ya kufa kwake? Unapomtazama Mwomkzi aliyeinuliwa, aliyesulubiwa na kubeba dhambi, utaruhusu matukio hayo yapenye moyoni mwako? Unapotafakari kwa kina uchungu wa kupitia mauti ya pili kwa niaba yako, utaruhusi hilo lifungue macho yako kuona uchafu wa dhambi unazozipenda? Ziungame kwa Yesu! Atakusamehe kwa furaha. Atakufariji. Na atakupatia ushindi.

Taarifa za Sifa:

- Diane T., anasema "Namshuru Mungu kwa fursa ya kuhudhuria kambi la Biblia liitwalo Virtual ARME Bible Camp! Kuna mibaraka mingi wakati huu."
- Iris R., anasema "Nilikuwa nimeathirika kwa uraibu wa kutazama sinema kupitia programu tumishi ya Netflix. Nilikuwa nasoma mafungu machache ya Biblia na kujaribu kujihesabia haki mwenyewe, na kisha niliendelea kutazama. Baada ya juma la maombi shuleni kwetu Mungu alinigusa nikafuta ile programu. Baada ya hapo nilirudia nikaanza kutazama sinema za Biblia, lakini sikuweza kujidhibiti, nilirudi tena na kuwa chini ya udhibiti wa Shetani. Nilimlilia Mungu. Siku iliyofuata mchungaji wangu alinizawadia Biblia toleo liitwalo Andrews Study Bible. Niliifurahia na nikamshukuru Mungu kwa machozi kwa kuingilia kati. Alinikumbusha Wafilipi 2:13 'Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.' Ninamsifu Mungu kwa kunishawishi na kwa kutimiza ahadi yake.'

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** uelewa wazi wa kile hasa kilichotokea msalabani**.** Omba kwa Mungu akusaidie kuichukia dhambi na kupenda haki.
- **Ombea** kazi ya Uinjilisti wa vitabu kule Malawi na msaada ya kifedha wa kuanzisha sanitarium na kazi ya umishenari kwa njia ya afya katika eneo lile.
- **Ombea** watu wasihamishwe kwenye mtari kwa nadharia za kibinadamu, bali wakaze macho yao kwa Yesu na ukweli wake.
- **Ombea** washiriki wa kanisa la Peter's Rest SDA kule St. Croix, Virgin Islands. Kanisa lao liliteketea kabisa kwa moto. Ombea hekima ya namna watakavyo songa mbele. Omba kwamba hasara hii igeuzwe kuwa ushindi katika Yesu.

Siku ya 60, Jumatatu, Mei 25, 2020

UPOLE UNAOLIPA

Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi- Mathayo 5:5

"Asili ya kibinadamu daima inapambana kwa ajili ya kujieleza, ipo tayari kupambana; lakini yeye ajifunzaye kwa Kristo anaondolewa ubinafsi, kiburi, kupenda ukuu, na rohoni mwake kuna ukimya. Ubinafsi unasalimishwa kwa utendaji wa Roho Mtakatifu, Kisha hatuna shauku ya kushika nafasi ya juu. Hatuna tamaa ya kujitukuza na kujitutumua ili tujulikane; bali tunajisikia kwamba nafasi yetu ya juu kabisa ni miguuni pa Mwokozi wetu. Tunamtazama Yesu, tukisubiri mkono wake utuongoze, na kuisikia sauti yake ili ituongoze." – Thoughts from The Mount of Blessing, p. 15

Maswali ya Moyoni: Hakuna mahali penye furaha maishani kama kujua kuwa una mwafaka na Mungu katika yote unayofanya. Mwafaka huu huwepo Yesu anapotafutwa, na kujiinua nafsi kunapoachwa, kwa kutambua kuwa "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha." (Yeremia 17:9). Unyenyekevu, upole ni ufunguo wa kumruhusu Roho Mtakatifu kukuza ndani yako, tabia maridadi ya kweli inayofanana na Kristo. Je! utamwomba Yesu akuondolee tamaa zako zenye kiburi, matakwa yenye kiini katika nafsi, kupenda ukuu? Unaweza kumwomba ayabadilishe hayo kwa kukuwezesha kuonesha kwa vitendo uungwana, upole, na unyenyekevu kuanzia leo?

Taarifa za Sifa:

- Claudia P., anasema "Ninamsifu Mungu kwani rehema zake za upole ni mpya si tu kila asubuhi, bali kila wakati! Amekuwa mwema kwa familia yangu na mimi zaidi ya maneno yanavyoweza kuelezea. Ninakusifu Mungu!"
- Rose K., "Msifu Mungu kwa ajili ya Siku 100 za Maombi! Kila siku ninasukumwa kufanya kitu kipya, au kuona mabadiliko mapya kwa waumini wengine. Baadaye nilitambua kuwa kile nilichokiona hakika lilikuwa ni jibu kwa mambo ya kuombea katika Siku 100 za maombi. Ni ajabu kuona namna Roho Mtakatifu anavyotenda kazi."

MAMBO YA KUOMBEA

- **Mwombe** Yesu akufanye uwe mnyenyekevu na mpole.

- **Waombee** washiri kule Uganda walioathirika kwa mafuriko ya hivi karibuni. Mafuriko yameacha nyumba nyingi zikiwa zimeharibika. Wengi sasa hawana nyumba katikati ya hali ya kuzuiliwa.

- **Waombee** walimu Waadventista ulimwenguni kote kwani wengi wanakabiliwa na mambo magumu ya kifedha kwani hawawezi kwenda kufanya kazi.

- **Ombea** vijana watambua umuhimu wa kumtumikia Mungu na sio ulimwengu.

Siku ya 61, Jumanne, Mei 26, 2020

LISHE YA HAKI

Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa – Mathayo 5:6

*"Hali ya haki ni utakatifu, kufanana na Mungu, na 'Mungu ni upendo' 1 Yohana 4:16. Ni kuifuata sheria ya Mungu, kwani '*maagizo yako yote ni ya haki.' *(Zaburi 119:172), na 'upendo ni utimilifu wa sheria' (Warumi 13:13). Hali ya haki ni upendo, na upendo ni nuru na uzima wa Mungu. Haki ya Mungu imo ndani ya Kristo. Tunapokea haki kwa kumpokea yeye."*– Thoughts from The Mount of Blessing, p. 18

Maswali ya Moyoni: Je! Una njaa na kiu ya haki ya Kristo? Maisha yake ya upendo kamili usio na ubinafsi na kifo chake badala yetu hukupatia zawadi yenye sehemu mbili za neema ya kuhesabiwa haki: 1.) Ahadi kwamba umefunikwa kwa maisha yake makamilifu kwa njia ya imani katika ile ahadi. 2.) Ahadi kwamba atakubadilisha kutoka kuwa kiumbe chenye ubinafsi, hadi kuwa kiumbe kinachoakisi upendo wa Yesu usio na ubinafsi, kwa njia ya imani hai iliyo katika ile ahadi. Ahadi hii yenye sehemu mbili itakukamilisha; itakuridhisha kwa hakika; itakuokoa! Kwa nini usiikubali leo na kuanza kuishi maisha ya furaha na yaliyojazwa na Yesu ukiwa na uelewa wa ukweli huu wa kushangaza wa upendo wa Mungu unaookoa?

Taarifa za Sifa:

- Jane D., anasema" Mungu alimponya mgonjwa niliyemwombea. Kwa namna ya ajabu pia aligusa mioyo ya watu wa familia yangu."
- Marcia N., anasema "Binti yangu amekuwa na uraibu wa madawa kwa miaka mingi, alikuwa hana makazi na hata alifungwa gerezani. Kikundi chetu cha maombi kilianza kumwombea na kama matokeo yake kwa sasa yupo kwenye kituo maalum akipokea msaada, afya yake inaimarika, ana shauku mpya kwa ajili ya Mungu, na anasoma vitabu vya Roho ya Unabii. Alisema ni Mungu aliyemsaidia. Ninamsifu Mungu kwa ajili ya upendo wake kwetu na kwa kutusaidia kupita katika miaka hii ya kuvunja moyo. Kilio hudumu kwa usiku mmoja, bali FURAHA huja asubuhi.!

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** haki ya Kristo ikufunike na kukujaza.

- **Omba** Mungu aingilie kati mripuko wa ugonjwa wa uti wa mgongo katika maeneo ya magharibi ya nchi ya Ghana. Mripuko huu umekwisha ua watu wengi katika maeneo mengi.

- **Ombea** makanisa ambayo yamepoa tangu kuingia kwa Covid-19. Ombea wachungaji, viongozi wa kanisa, na washiriki kujua namna bora ya kuwa na mwunganiko wakati huu. Ombea kuwe na lengo jipya kwa umuhimu wa maombi.

- **Ombea** washiriki katika nchi ya Myanmar wanapoendelea kutumia mtandao kueneza injili katika nyakati hizi za zahama.

Siku ya 62, Jumatano, Mei 27, 2020

UWE NA REHEMA!

Heri wenye rehema; Maana hao watapata rehema – Mathayo 5:7

"Mungu mwenyewe ndiye chanzo cha rehema yote. Jina lake ni la 'rehema na neema' (Kutoka 34:6). Hatutendea sawa sawa na udanganyifu wetu. Hatuulizi iwapo tunasustahili upendo wake, lakini humwaga juu yetu utajiri wa upendo wake, ili kutufanya tustahili. Hana kisasi. Hatafuti kuadhibu, bali kukomboa... anatamani, kwa shauku kuu, kulegeza ole za wanadamu na kupaka mafuta majeraha yao...Wenye rehema ni 'washirika wa asili ya uungu,' na ndani yao upendo wa Mungu wenye huruma unaonekana. Wote ambao mioyo yao ina huruma pamoja na moyo wenye upendo wa milele watatafuta kurejesha na sio kuhukumu. Kristo akaapo ndani ya roho ni chemi chemi isiyo kauka kamwe. Anapokaa, patakuwa na furiko la wema." – Thoughts from The Mount of Blessing, p. 22

Maswali ya Moyoni: Tenga muda na utafakari kuhusu rehema ya Mungu maishani mwako. Anakutakia mema tu, hata kama wewe sio mwaminifu. Hakutaki umthitishie thamani yako kwake ndipo upokee karama yake ya wokovu. Anakutendea kwa upendo.
Unapopata uzoefu na kuipokea rehema ya Mungu, Roho Mtakatifu atakuwezesha kuwa wakala wa rehema; akiwatendea wale wote wanaokuzunguka kwa upendo ule ule na rehema. Na hasa wale waliokukosea. Je! utachagua leo, kwa msaada wa Yesu, kuwapa watu rehema ya Mungu maishani mwako? Kuwasamehe kabla hawajaomba msamaha, kuwa penda kabla ya kupata sababu ya kuwapenda? Kuwatakia mema bila kujali kama wanastahili au la?

Taarifa za Sifa:

- Elham L., anasema "Nimekuwa nikimwomba Mungu ili niwe na uhusiano wa kina pamoja naye. Tangu nianze kushiriki Maombi ya Siku 100 kila siku maisha yangu ya maombi yametiwa nguvu. Yanashangaza!"
- Sherma J., anasema "Mungu alijibu ombi kwa ajili ya mshiriki aliyepotea. Nilipojaribu kumpigia simu alipuuzia. Nilipomtembelea alikuwa akiongelea matatizo tu na hakuniruhusu mimi kusema cho chote. Nilimwomba Mungu auguse moyo wake na badala ya mimi kujaribu kumpigia yeye ndiye anipigie simu. Majuma mawili baadaye alinipigia na kuniambia kuwa matatizo yake yametoweka na anahitaji kurudi kanisani na kuyatoa maisha kwa Mungu!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** Mungu akufanye kuwa wakala wa rehema kwa watu maishani mwako.
- **Ombea** wanafunzi wanaohangaika kupata ada ya shule ili kupata elimu. Omba ili waone uongozi wa Mungu katika elimu yao.
- **Ombea** watu na washiriki wa Zimbabwe. Wengi wao hawawezi kukaa chini ya zuio la kutotoka nje. Mfumo wa afya hauna uwezo wa kukabiliana na zahama ya Covid-19.
- **Ombea** wachungaji kadhaa nchini Indonesia walioambukizwa Covid-19.
- **Omba** Mungu kwa ajili ya programu ya ushuhudiaji ya wanafunzi nchini Brazil wanaojitolea kutengeneza dawa za kusafishia mikono kwa ajili ya wazee.

Siku ya 63, Alhamisi, Mei 28, 2020

MOYO SAFI

Heri wenye moyo safi; Maana hao watamwona Mungu – Mathayo 5:8

"Roho Mtakatifu huuchukua ukweli kuhusu Mungu na yeye aliyemtuma, na kuufunua kwenye ufahamu na moyoni. Walio safi moyoni wanamwona Mungu katika uhusiano mpya na wakupendeza, kama Mkombozi wao; na wanapotambua usafi na upendo wa tabia yake, wanatamani kuakisi sura yake. Wanamwona kama ni Baba anayetamani kumkumbatia mtoto wake anayetubu, na mioyo yao inajazwa furaha isiyotamkika na utukufu tele."
– Thoughts from The Mount of Blessing, p. 26

Maswali ya Moyoni: Tunapotembea na Mungu kwa uaminifu, yeye daima hufungua macho yetu kwenye ufahamu zaidi na zaidi wa tabia yake ya upendo, mapenzi yake, na uzuri wake. Katika utambuzi wa utakatifu wake kamili na usafi, uchafu wetu unakaribia nuru na tunaalikwa kupokea utakaso ambao ni yeye pekee awezaye kutoa. Kwa upande huu wa mbingu, tunaona kwa jicho la imani, lakini siku moja hivi karibuni, tutamwona uso kwa uso! Hiyo itakuwa ni siku yenye utukufu. Kwa nini tusimwombe aitakase mioyo yetu dhidi ya uchafu wote na unajisi? Kwa nini tusitafute moyo safi kwa vitendo na kumfahamu Mungu wetu na mapenzi yake.?

Taarifa za Sifa:

- Shana S., anasema "Wakati wa Siku 100 za Maombi nilianza kumwombea rafiki yangu mwenye miaka 20 ambaye mwaka 2017 alianza kunipuuza bila sababu. Alizuia jina langu kwenye simu yake. Nilijitahidi kumpigia mara nyingi. Hakuna jibu. Siku ya pili alinipigia! Aliniunganisha tena akaniambia sikumfanyia kosa lo lote. Tuliungana tena na kupatana. Mungu hujibu maombi yetu.!"
- John K., anasema "Hapa Uganda amri ya kutotoka nje imeacha wengi wakiwa na njaa. Wakati wa vipindi vya Siku 100 za Maombi Mungu alinipatia hekima ya kuwasaidia watoto wenye njaa.
- Niliziandikia ujumbe familia100 toka kanisani na kuwaomba wawapatie chakula watu wenye njaa walio karibu nao. Wazo hili rahisi lilienea katika eneo zima kupitia mwandishi wa habari aliyelirusha mtandaoni. Kwa mwunganiko mpya tulianzisha mikutano ya uinjilisti kwa njia ya mtandao wa WhatsApp.!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kwa ajili ya moyo safi, ulio huru dhidi ya dhambi, moyo uliotakaswa dhidi ya uchafu wote.
- **Ombea** watu wanaushughulikia mazishi na huduma za kuhufadhi maiti kwani wanashughulika moja kwa moja na watu waliokufa kwa Covid-19.
  Ombea kanisa kule Fiji, wanapofikiria kufanya mabadiliko ya kimfumo na kuwaimarisha walei katika kushika wa baadhi ya majukumu
- **Ombea** huduma ya Kanisa la Harvest SDA kule Alabama, Marekani. Wapo kwenye eneo la watu wa kipato cha chini, uhalifu ni mwingi, na wameona matunda kidogo mno ya juhudi zao za kuokoa roho. Omba ili Mungu aingilie kati.